

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

MKOA WA RUVUMA

Simu Nambari. 025-2602256/2602238

Fax No. 2602144

E-mail. rasruvuma@pmoralg.go.tz



Ofisi ya Mkuu wa Mkoa,
S. L. P. 74,
SONGEA.

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Mheshimiwa Dkt. Binilith Satano Mahenge ameagiza wananchi wote wa Mkoa wa Ruvuma kuwa kuanzia leo tarehe 21 Aprili, 2017 ni Marufuku wakulima kuuza mashamba yao yenye mahindi mabichi kwa bei ya jumla au rejareja kwa nia ya kuyasafirisha kwenda nje ya Mkoa wa Ruvuma kwa lengo la kufanya biashara ya mahindi ya kuchoma.

Amesema Mwananchi yeyote atakayekamatwa akisafirisha mahindi mabichi nje ya Mkoa atachukuliwa hatua kali za kisheria.

Lengo la marufuku hii ni kuwawezesha wananchi kutunza mashamba yao hadi msimu wa mavuno wa zao la mahindi utakapofika na kuziwezesha kaya kuwa na uhakika wa chakula.

A handwritten signature in blue ink, appearing to read 'Revocatus A. Kassimba'.

Revocatus A. Kassimba
AFISA HABARI – OFISI YA MKUU WA MKOA
RUVUMA
21 Aprili, 2017